# Askari wanaokiuka haki za wanyama kukiona

Na Peti Siyame, Sumbawanga

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema serikali haitasita kuwachukulia hatua kali askari wahifadhi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori nchini (TAWA) wanaokiuka haki za wanyama.

Alibainisha hayo alipozungumza na wafugaji katika wilaya za Nkasi na Sumbawanga mkoani Rukwa akiwa katika ziara ya siku tatu ya kikazi mkoani humo iliyohitimishwa jana.

Katika mazungumzo hayo, wafugaji walilalamika kuwa, baadhi ya askari wa TAWA wanawakamata wakitoka kununua ng'ombe au kuwapeleka minadani wakiwapitisha kwenye barabara zinazopita hifadhini.

Mmoja wa wafugaji wilayani Nkasi, Gia Sai, alisema: "Wakiwakamata wanawatelekeza hawapati malisho wala matibabu hatimaye wanakufa. Pia tunapigwa..."

Akizungumzia suala hilo, Ndaki alisema: "Hii inasikitisha mbona sasa barabara zimejengwa zikipita ndani ya hifadhi isitoshe wanapowaamuru wafugaji wasafirishe mifugo yao kwa magari makubwa, haya magari makubwa yatapita wapi si kwenye hizo barabara?" alihoji.

Alisema atazifikisha tuhuma hizo kwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk Damas Ndumbaro ili hatua kali zichukuliwe dhidi ya askari wanaobainika kuhusika na vitendo hivyo.

"Baadhi ya hawa askari wa TAWA wanakiuka haki za wanyama kwani zipo taarifa za uhakika kuwa wanapokamata ng'ombe wa wafugaji wanawashikilia kwa muda mrefu bila kuwahudumia ipasavyo."

"Kutokana na wanyama hao kukosa huduma muhimu zikiwemo za malisho na chanjo, wengi wanakufa, hili halikubaliki ni ukiukaji mkubwa wa haki za wanyama," alisema.

Kuhusu uvalishaji hereni kwa mifugo, Waziri Ndaki aliwahimiza wafungaji wachangamkie fursa hiyo ili kulinda ubora wa ngozi za mifugo yao.

Alisema uvalishaji hereni ili kuhifadhi kumbukumbu kielektroniki, utarahisisha utambuzi, usajili na ufuatiliaji na serikali kuwa na idadi sahihi ya mifugo iliyopo nchini.

Alisema serikali imepiga marufuku mifugo kupigwa chapa ya moto kwa kuwa inasababisha mateso maumivu makali kwa mifugo na kuharibu ubora wa ngozi, hivyo kukosa soko la uhakika na lenye ushindani kitaifa na kimataifa.

Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo nchini, Profesa Hezron Nonga alisema katika kipindi cha 2015/16 na 2016/17 ng'ombe 17,000,000 walipigwa chapa ya moto kwa ajili ya utambuzi.

"Lakini robo tatu ya ng'ombe hao chapa zao zilifutika baada ya miezi mitatu," alisema.

Aliongeza kwamba asilimia 90 ya ngozi za mifugo nchini zinakosa soko kutokana na kutokuwa na ubora unaotakiwa kutokana na kupigwa chapa ya moto.

Alisema takwimu zilizopo zinaonesha kuwa nchini kuna ng'ombe wapatao milioni 38, mbuzi milioni 26 na kondoo milioni tisa.

Scanned with CamScanner

# Mifugo wafunga machinjio ya punda

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA *ya Mifugo na Uvuvi imeyafungia kwa muda machinjio ya punda yaliyoko Ibadakuli katika Manispaa ya Shinyanga, kutokana na kutoridhishwa na jinsi yanavyoendeshwa na hali ya usafi.*

Wizara imesema uchunguzi zaidi wa suala zima la machinjio hiyo utafanywa na kikosi maalumu kitakachopelekwa Shinyanga na kwamba ikibidi machinjio hayo yatafungiwa moja kwa moja.

Katika barua iliyosainiwa na Dk B.L.Malinda kwa niaba ya Katibu Mkuu wa wizara hiyo, imeelezwa kwamba kuna mapungufu mengi kuanzia upakiaji, usafirishaji wa punda kwenye malori kwa umbali mrefu huku wakipata majeraha, hadi namna ya kuchinja ambayo haizingatii haki za mifugo.

Wizara imeeleza kwamba imefuta ruhusa kwa Fang Hua Investment Co. Limited iliyotumiwa barua hiyo wiki iliyopita iliyotolewa Aprili mwaka huu, lakini tangu wiki iliyopita, kampuni imezuiwa kuingiza punda zaidi kwenye machinjio, bali kumaliza wale tu waliokuwa tayari ndani ya eneo lao.

Wizara imeeleza kwamba uchunguzi ukikamilika utatoa msingi wa uamuzi wa mwisho juu ya machinjio hayo yanayodaiwa kuchinja idadi kubwa zaidi ya iliyokubaliwa kwa siku ya punda 20. Timu ilikuwa ipelekwe pia kusimamia hatua za usitishaji wa uchinjwaji wa punda huko.

Timu za awali za wizara za ukaguzi kwenye machinjio hayo ziliwasilisha wizarani taarifa zinazoonesha kwamba operesheni kwenye machinjio hayo haziendi kwa mujibu wa maagizo yaliyokubaliwa na pande mbili hizo.

Daktari wa Mifugo anayesimamia machinjio hayo, Dk Isaya Gabriel alisema jana kwamba maelekezo ya barua hiyo yalipokewa na kutekelezwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Kutetea Haki za Mifugo Arusha (ASPA), Livingstone Masija alipongeza uamuzi huo wa serikali na kuomba ikiwa inawezekana uchinjaji wa punda upigwe marufuku moja kwa moja.

Masija alitoa sababu za rai yake kuwa punda ni rasilimali muhimu kwa kazi kama ubebaji mizigo na ukokotaji wa matela, hasa kwenye jamii za wafugaji na kwenye mikoa yenye ukame.

Alisema kwamba wakati punda mmoja huuza Sh 200,000 tu, kwa siku mnyama huyo akifanya kazi humwingizia mmiliki kati ya Sh 20,000 na Sh 50,000, kima ambacho ni kikubwa na kingemzalishia kiasi kikubwa cha fedha kwa wiki, mwezi na mwaka.

Ruhusa iliyotolewa na wizara katika kuchinja punda ilikuwa na masharti kadhaa, yakiwamo kampuni kusaidia kuwezesha kuanzishwa kwa mashamba binafsi ya kimkataba ya uzalishaji wa punda kuanzia 2018, jambo ambalo halijafanywa.

Masharti mengine ni kila kampuni kuanzisha programu 50 za uhamilishaji kwa kutumia mbegu kutoka koo safu zenye sifa hitajiwa kuanzia Desemba 2018. Ilikubaliwa pia kampuni zenyewe kuanzisha mashamba yake ya kitovu cha kuzalisha punda mwaka huo huo.

Kampuni ilitakiwa kuwa na punda 250 Agosti 2018 na 683 ifikapo mwisho wa mwaka wa nne; kuagiza majike 50 ya koo safu zenye sifa tajwa kutoka China kwa ajili ya kuzalisha punda zaidi na kufanya utafiti wa idadi ya punda katika halmashauri zote zilizopewa ruhusa ya kuchinja mnyama huyo.



Mw
wa
Mpi

Scanned with CamScanner